

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**  
**SHULE YA SEKONDARI SANGAMBI**  
**FOMU YA MAELEKEZO YA KLIJUNGA NA SHULE**

- i) Ndugu:.....ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha kwanza kuanzia mwaka wa masomo wa.....**HONGERA SANA**. Shule itafunguliwa tarehe.....unatakiwa kuripoti tarehe.....bila kuchelewa
- ii) Shule inapatikana katika Mji wa Sangambi **km 1 1/2** kutoka makao makuu ya ofisi ya kata na **km 15** kutoka barabara kuu inayotoka Mbeya kwenda Chunya. Aidha ukifika stendi ya Sangambi chukua usafiri wa piki piki au Bajaji kuelekea barabara ya Shoga utakikuta kibao cha shule upande wa kulia kinachoelekeza upande shule ilipo. Ukitokea Mbeya shukia kituo kinachojulikana njia panda ya Sangambi.

iii) **SARE YA SHULE**

Shule hii ni ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana sare zitakuwa kama ifuatavyo

a) **WASICHANA:-**

- Sketi mbili rangi ya orange kwaajili ya kuvaa darasani
- Sketi mbili rangi ya kijani kwaajili ya shughuli za nje
- Truck suit rangi ya blue kwaajili ya michezo
- T-shirt pea 2 rangi ya orange kwaajili ya shughuli za nje
- Sox pea 4 nyeupe kwaajili ya darasani
- Viatu pea 2 vyeusi vya kamba kwaajili ya darasani
- Raba pea 2 kwaajili ya michezo(rangi yoyote)
- Sweta 2 rangi damu yam zee za darasani kwa ajili ya baridi
- Nguo zingine za ndani ni muhimu kumnunulia (pads 5)
- Jacketi jeusi la kumkinga na baridi anapokuwa nyumbani
- Waislam wanaruhusiwa kuvaa hijabu nyeupe kichwani (ndefu)

b) **WAVULANA:-**

- Suruali mbili rangi ya orange kwaajili ya kuvaa darasani
- Suruali mbili rangi ya kijani kwaajili ya shughuli za michezo
- Truck suit rangi ya blue kwaajili ya michezo
- T-shirt rangi ya orange pea 2 kwaajili ya kazi za nje
- Sox pea 4 rangi nyeupe kwaajili ya kuvaa darasani
- Viatu pea 2 vyeusi vya kamba kwaajili ya kuvaa darasani
- Raba pea 2 rangi yoyote kwaajili ya michezo (za kamba)
- Sweta pea 2 damu ya mzee kwaajili ya darasani ili kujikinga na baridi
- Nguo zingine za ndani muhimu
- Jacket jeusi kuwakinga na baridi wanapokuwa nyumbani

NB: sare hizi zitatumika kuvaliwa shuleni na nyumbani mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa nguo nyingine yoyote kwa muda wote akiwa mwanafunzi wa shule, iwe weekend, likizo au muda wowote hadi anamaliza kidato cha nne.

